

Yule aliyemzuia Yohana asimsujudie alikuwa ni Mwanadamu au
Malaika?

Yule aliyemzuia Yohana asimsujudie katika Ufunuo 19:10 alikuwa ni nani, Je!
ni Mwanadamu au Malaika?

JIBU: Tusome...

*Ufunuo 19: 10 “ Nami nikaanguka mbele ya miguu yake, ili
nimsujudie; akaniambia, Angalia, usifanye hivi; mimi ni mjoli
wako na wa ndugu zako walio na ushuhuda wa Yesu. Msujudie
Mungu. Kwa maana ushuhuda wa Yesu ndio roho ya unabii”.*

Mtu anayetumika kama wewe huyo ni Mjoli wako. Mfanyakazi anayefanya
kazi kama ya kwako huyo ni mjoli wako na wewe ni mjoli wake...Hivyo katika
Mstari huo hapo juu Yohana alikuwa anataka kumsujudia yule aliyekuwa
anazungumza naye, aliyekuwa anamwonyesha maono yale...Lakini akamzuia
na kumwambia mimi ni mjoli wako (maana yake ninayafanya kazi kama ya
kwako ya utumishi)..na pia wa ndugu zako (yaani wanadamu wenzake ambao
ndio sisi tulio na ushuhuda wa Yesu).

Malaika ni wakina nani?

Kwasababu Biblia inasema Malaika ni roho watumikao..wanaotuhudumia
sisi(Soma Waebrania 1:3-14)..Kadhalika na sisi wanadamu tunaomtumikia
Mungu ni Watumishi wa Mungu vile vile...tunaotumika katika Ufalme wa

Yule aliyemzuia Yohana asimsujudie alikuwa ni Mwanadamu au
Malaika?

Mbinguni..Hivyo sisi pamoja na malaika ni Watumishi wa Mungu wa mbinguni...Kwahiyo sisi ni wajoli wa Malaika na Malaika vile vile ni wajoli wetu.

Kwahiyo tukirudi kwenye hilo swalii linalouliza.. “aliyemzuia Yohana asimsujudie alikuwa ni Mwanadamu au Malaika?”...Jibu lake ni kwamba alikuwa ni MALAIKA. Kwasababu Yohana tangu mwanzo alikuwa haonyeshwi maono yale na mwanadamu yoyote...bali Malaika ambaye naye huyo Malaika aliyapokea maono hayo kutoka kwa Yesu Kristo mwenyewe. Hakuna mwanadamu yoyote aliyejhuisika hapo kwa namna moja au nyininge..

Ufunuo 1:1 “Ufunuo wa Yesu Kristo, aliopewa na Mungu awaonyeshe watumwa wake mambo ambayo kwamba hayana budi kuwako upesi; naye akatuma KWA MKONO WA MALAIKA akamwonyesha mtumwa wake Yohana”

Wapo watu wanakosa shabaha katika hilo kudhani kuwa Yule alikuwa ni mtakatifu Fulani aliyekufa zamani au aliyepaa pengine Musa au Eliya, au Nabii Fulani, kwamba ndiye aliyemwambia maneno hayo asimsujudie kwa kuwa yeye ni mjoli wake na wa ndugu zake walio na ushuhuda wa Yesu. Japo ambalo si la kimaandiko..Lakini sasa tunajua kuwa yule hakuwa mwanadamu bali ni Malaika wa mbinguni.

Yule aliyemzuia Yohana asimsujudie alikuwa ni Mwanadamu au
Malaika?

jiunge na channel yetu Kwa kubofya hapa >> **WHATSAPP**

Bwana akubariki.

Maran atha!

Mada Nyinginezo:

UFUNUO: Mlango wa 19

DANIELI: Mlango wa 1

ESTA: Mlango wa 1 & 2

Uasherati wa Kiroho maana yake nini?

Yule aliyemzuia Yohana asimsujudie alikuwa ni Mwanadamu au
Malaika?

*ALIKUWAKO NAYE HAYUKO, NAYE YU TAYARI KUPANDA KUTOKA
KUZIMU.*

Rudi Nyumbani:

Share on:

WhatsApp